
Bilde: Mostphotos

# Ungependa kushiriki katika mpango wa mwongozo wa wazazi?

**Kila mtu anataka kuwa mzazi mzuri kwa watoto wake. Kuwa mzazi katika nchi ya kigeni inaweza kuwa changamoto. Tungependa kukualika wewe na familia yako kujiunga na mradi wa utafiti kuhusu mwongozo wa wazazi. Tunatafuta familia ambazo zimekuwa wakimbizi na sasa zinaishi Norway na watoto wenye umri wa miaka 6-12.**

## UTAFITI HUU UNAHUSU NINI?

Kuimarisha ujuzi wenu kama wazazi na kuboresha mwingiliano na watoto wenu.
Ili kujua ikiwa mwongozo wa wazazi unaweza kusaidia familia za wakimbizi.

## KUSHIRIKI KUNAHUSISHA NINI?

Utashiriki katika moja ya programu hizi za mwongozo wa wazazi (watu watagawanywa katika vikundi bila mpangilio):

- Programu ya Kimataifa ya Maendeleo ya Watoto (ICDP), kozi ya mwongozo wa wazazi inayodumu kwa wiki 12.
- Miaka ya Ajabu (DUÅ), kozi ya mwongozo wa wazazi inayodumu kwa wiki 15.

Kila mtu anayeshiriki ataulizwa kujaza fomu ya maswali. Baadhi ya familia pia zitachaguliwa kushiriki kwenye mahojiano. Nusu ya familia zitaulizwa kutoa maoni, kwa kutumia App kwenye smartphone zao.
*Habari yote tunayopata kuhusu wewe itakuwa ya siri.*

## FAIDA ZA KUSHIRIKI

Utashiriki katika mpango wa mwongozo wa wazazi kwa msingi wa kikundi (DUÅ/ ICDP). Utakutana na wazazi wengine kwenye mikutano ya kikundi ambao unaweza kubadilishana nao uzoefu wako. Lengo ni kumsaidia mama au baba ahisi salama zaidi katika jukumu lao kama mzazi kwa kufahamu zaidi njia bora ya kulea mtoto. Utapokea zawadi baada ya kujibu fomu ya maswali ya tatu na ya nne.

## NANI ANAWEZA KUSHIRIKI?

Familia zilizo na watoto wenye umri wa miaka 6-12 ambao walihamia Norway ndani ya miaka tisa iliyopita.

## UNASHIRIKI VIPI?

Tazama maagizo nyuma ya brosha hii.

# JINSI YA KUTOA IDHINI YA KUSHIRIKI KATIKA UTAFITI
## Unaweza kutoa idhini kwa kujaza fomu kwenye karatasi ama mtandaoni

### Jinsi ya kutoa idhini mtandaoni:

- **Nenda kwa tovuti ya utafiti wa PIRM: https://uit.no/forskning/pirm**
- **Bonyeza "Idhini" katika lugha unayopendelea. Unaweza kuchagua kati ya Kinorwe, Kiingereza, Kisomali, Kiarabu, Kifaransa, Kiswahili, Kituruki na Kitigrinya**
- **Ingia tovuti ukitumia ID-porten**
- **Soma habari kabla ya kutoa idhini yako ya kushiriki kwenye utafiti**
- **Jaza taarifa ya mawasiliano na uitume**

**Kwa idhini kwa karatasi, tafadhali wasiliana na ofisi ya huduma iliyo karibu nawe kwa usaidizi.**

### Mtu wa kuwasiliana naye ni: ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___

___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___ ___

Mmoja wa wafanyakazi wa mradi atawasiliana na wewe kabla ya mradi kuanza. Taarifa zote tunazokusanya zitawekwa kwa usalama na kuchungwa kwa siri sana. Ushiriki wako kwenye utafiti ni kwa hiari na unaweza kujiondowa wakati wowote. Kushiriki katika utafiti HAKUTAKUWA na ushawishi wowote kwa faida zingine au msaada unaopokea kutoka kwa huduma za afya.

Ikiwa una maswali yoyote ama unataka kuuliza mambo mengine kuhusu utafiti, kuwa huru kuwasiliana nasi:

RKBU Nord, kwa mratibu wa mradi Joshua Patras kwa barua pepe: pirm@uit.no au kwa kupiga simu: 77 64 62 65

UiT RKBU Nord

KAVLI FONDET

NORCE

NTNU
Regionalt kunnskapssenter
for barn og unge
– Psykisk helse og barnevern

Bufetat

Regionsenter for barn og unges psykiske helse
Helseregion Øst og Sør